

# Huduma Zinazopatikana DVR

DVR inatoa huduma mbalimbali ili kukusaidia kujiandaa, kupata na kudumu kwenye kazi. Huduma unazopata zinategemea na mahitaji na mazingira yako binafsi. DVR inaweza kukupa taarifa muhimu ili kukusaidia kuamua ni huduma gani unazihitaji ili kufikia lengo la kazi yako. Zinajumuisha:

**Huduma za tathmini** ili kupima vipaji vyako, uwezo wako, stadi za kazi, na mapendeleo yako na kukusaidia katika kuchagua lengo la kazi na huduma za usadizi za DVR unazohitaji ili kufikia lengo hilo.



**Huduma za upangaji wa mafao** ili kukusaidia kuelewa jinsi suala la kufanya kazi linavyoweza kuathiri fedha taslimu za ulemavu au mafao ya tiba (k.m., Kipato cha Huduma za Ziada au Bima ya Huduma za Kijamii za Ulemavu) ambazo unapokea.

**Huduma za ushauri na mwongozo** zinazotolewa katika kipindi chote cha mchakato wa urekebishaji ili kukusaidia kufanya maamuzi mazuri kuhusu namna ya kufikia lengo lako.

**Huduma za maisha ya kujitegemea** ili kukusaidia kuelewa changamoto za ulemavu zinazokuzuia wewe kufanya kazi. Zinajumuisha, lakini hazikomei kwa:

- Mafunzo ya kujihudumia
- Usimamizi wa fedha
- Kutumia usafiri wa umma

**Huduma za teknolojia saidizi** ili kukusaidia kuondoa vizuizi vya mawasiliano na/au kimwili vinavyoweza kukuzuia kupata na kudumu kwenye kazi unayoitaka. Zinaweza kujumuisha vifaa kama vile visaidizi vya kusikia, visaidizi vya kuona, au programu maalum ya kompyuta. Unaweza kuangalia pamoja na mshauri wako jinsi teknolojia inavyoweza kukusaidia kufikia lengo la ajira yako.

**Mafunzo au elimu** ili kukusaidia kujenga stadi na kukidhi sifa za kazi.

**Huduma za kutafutiwa kazi** ili kukusaidia kufanya utafutaji wako wa kazi, ikiwemo:

- Usaidizi wa kujaza maombi ya kazi
- Kuandaa tawasifu (resume)
- Kufanya mazoezi ya stadi za usaili, na kutambua dondoo za kazi



## Dhima

Kubadilisha maisha kwa kuwasaidia watu wenye ulemavu kushiriki kikamilifu kwenye jumuiya zao kupitia ajira zenye tija.

## Dira

Wataalamu wenye kujitua ambao ni viongozi katika nyanja ya urekebishaji kupitia ufundi, kutoa uzoefu wa kipekee kwa kila mteja, kila wakati.

## Maadili

- **Uwazi** kupitia mawasiliano yaliyo dhahiri na yanayozingatia uaminifu kwa wateja, wafanyakazi, na wabia
- Kutenda kwa **uadilifu**, kusimamia maadili na kanuni za taaluma yetu.
- Kuendeleza utamaduni wa **Uwezeshaji** kwa wateja na wafanyakazi
- Kuendeleza shughuli za urekebishaji kupitia **Uvumbuzi**
- **Ushirikiano** pamoja na wateja, wafanyakazi, na wabia wanaoleta matokeo.
- Kuazimia katika **Uanuwai, Usawa**, na **Ujumuishaji** katika miundo yake yote ili kufikia ubora.

Division of Vocational Rehabilitation  
Washington State Department  
of Social and Health Services  
PO Box 45340 • Olympia, WA 98504-5340  
1-800-637-5627  
Washington Relay: 711  
dshs.wa.gov/dvr

Inatoa Huduma za DVR Tangu 1933

Fedha za Jimbo na Serikali Kuu zinatumiwa kufikisha huduma za DVR. Programu ya VR inapokea takribani asilimia 78 kutoka fedha za Serikali Kuu na asilimia 22 kutoka fedha za jimbo. Kwa taarifa za kina kuhusu kiasi cha dola za fedha za Serikali Kuu kwa ajili ya programu hii, tafadhali tembelea <https://rsa.ed.gov/programs.cfm?pc=basic-vr&sub=awards>.

# Tumia Uwezo Wako



*Divisheni ya Urekebishaji Kupitia Ufundi*

# Je, DVR ni sahihi kwako?

## Kuhusu DVR

DVR ni rasilimali inayopatikana jimboni kote inayowasaidia watu wenye ulemavu kujiandaa, kupata, kudumu, kuendelea, au kupata tena ajira. DVR inashirikiana na mashirika na makampuni ili kutengeneza fursa za ajira.

## DVR inamhudumia nani

Watu wanaotafuta ajira yenye tija na iliyo thabiti lakini ulemavu wao unaweza kusababisha kizuizi kimoja au zaidi katika kufikia lengo la ajira.

## DVR inaweza kukusaidia kwenda kazini

Wafanyakazi wa DVR watakusaidia kupata taarifa unazohitaji ili kufanya uamuzi sahihi kuhusu:

- Aina gani ya kazi unayohitaji
- Hatua zinazohitajika ili kufikia lengo la kazi yako

Kwa usaidizi wa DVR, utaweza:

- Kubuni na kutekeleza mpango wa hatua kwa hatua ili kufikia lengo la ajira yako



# Mchakato wa Urekebishaji

## Maombi

- DVR itakupa taarifa zinazohusu huduma za urekebishaji kupitia ufundi.
- Unapaswa kutuma maombi kwenda kwa DVR kabla ya huduma kuanza.
- Maombi yako yatapitwa na mshauri wa DVR li kubaini kama unastahiki huduma za DVR.



## Ustahiki

Unastahiki huduma za DVR ikiwa:

- Una ulemavu wa kimwili, kiakili, au ufahamu unaoleta kizuizi katika ajira;
- Unahitaji huduma za urekebishaji kupitia ufundi ili kupata au kubaki kwenye kazi; na
- Una uwezo wa kufanya kazi baada ya kupata huduma za DVR.

Timu yako ya ushauri wa masuala ya DVR inakusanya rekodi ili kufuatilia utambulisho wako, ulemavu wako, na hali yako ya kazi. Kama hakuna rekodi za ulemavu wako, unaweza kuhitajika kufanya uchunguzi au vipimo vya kitiba ili kuthibitisha au kutetea ustahiki wako.

## Orodha ya Kusubiri

Kama DVR haiwezi kumhudumia kila mtu mwenye ustahiki kwa sababu ya vizuizi vya kifedha, lazima iandae orodha ya kusubiri huduma. Kisheria, DVR inapaswa kutoa kipaumbele cha huduma kwa watu wenye ulemavu mkubwa zaidi.

Watu watachaguliwa kutoka kwenye orodha ya kusubiri kutokana na ukubwa wa ulemavu wao na tarehe waliyotuma maombi ya huduma. Mshauri wa DVR atabaini ukubwa wa ulemavu na kipengele cha kipaumbele na kukutaarifu ubainifu huu kama sehemu ya mchakato wa ustahiki.

## Tathmini ya Ufundi

Wewe na mshauri wako wa DVR mtaangalia aina za kazi zinazoendana na tathmini yako ya ufundi. Mtafanya mapitio ya:

- Vipaji, uwezo na mapendeleo yako;
- Historia yako ya kazi na stadi; na
- Taarifa kuhusu mielekeo ya soko mahalia la kazi.

Au unaweza kukamilisha:

- Mitihani ya mapendeleo na/au umahiri, au
- Majaribio ya kazi.



## Mpango wa Ajira

Mshauri wako wa DVR anatoa ushauri na mwongozo endelevu ili kukusaidia wewe katika uandaaji wa Mpango wako Binafsi wa Ajira (IPE). Hii inajumuisha:

- Kuchagua lengo la kazi;
- Kuanisha ni hatua na huduma gani unazohitaji ili kufikia lengo la kazi yako; na
- Kufanyia kazi shughuli zilizoanishwa kwenye mpango wako. Zinaweza kujumuisha:
  - Mafunzo na elimu
  - Kufanya utafiti wa kazi
  - Kutafiti rasilimali na rufani zinazohusiana na kazi husika
  - Mafunzo ya kutafuta kazi
  - Mbinu za tawasifu (resume) na usaili
  - Usaidizi wa kutafutiwa kazi
  - Usaidizi wa kudumu kwenye kazi

## Kufanikiwa Kuajiriwa

- Baada ya kupata kazi, DVR itadumisha mawasiliano nawe kwa angalau siku 90 ili kuhakikisha kwamba kazi husika inakufaa.
- Baada ya siku 90, kama unaendelea vizuri kwenye kazi na hakuna huduma nyingine zinazohitajika, wewe na mshauri wako wa DVR mtaamua lini mfunge faili lenu.

## Baada ya Ajira

- Kama unahitaji msaada baada ya faili lako kufungwa na ilhali umefanikiwa kuajiriwa, DVR inaweza kufungua tena faili lako na kutoa usaidizi ili kukusaidia kudumu kwenye kazi yako.
- Kama utapoteza kazi yako, DVR inaweza kukusaidia kuomba tena huduma za DVR na inaweza kukusaidia kupata kazi kama hiyo.